



TAARIFA KWA UMMA

TANZIA



Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. William A. L. Anangisye, anasikitika kutangaza kifo cha **Prof. Hudson H. Nkotagu (1956-2021)**, kilichotokea tarehe 31 Agosti 2021 katika Hospitali ya TMJ, Dar es Salaam.

Marehemu **Prof. Nkotagu** alikuwa Profesa Mshiriki wa Jiolojia na Sayansi ya Mazingira katika Idara ya Jiolojia, Shule Kuu ya Madini na Jiosayansi. Alianza kazi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama Mhadhiri Msaidizi mwaka 1986. Alipanda vyeo vya kitaaluma hadi kufikia ngazi ya Profesa Mshiriki mnamo mwaka 2013, cheo alichokuwa nacho hadi alipofariki.

**Prof. Nkotagu** alikuwa msomi na mwanataaluma mbobezi aliyetafiti, kuchapisha na kushauri katika maeneo ya jotoardhi, nishati, haidrojiolojia na sayansi za mazingira. Prof. Nkotagu alitoa machapisho mengi katika majarida yanayoheshimika duniani. Alishiriki katika kazi mbalimbali za ushauri ndani na nje ya nchi ikiwemo kuandaa Ramani ya Afrika ya Haidrojiolojia nchini Ufaransa akiwakilisha Tanzania. Aidha, alikuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Maji ya Taifa, Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Chuo cha Madini, mratibu wa mafunzo wa masuala ya mazingira Maziwa Makuu yaliyopo katika nchi za kitropiki za Afrika hususani kwenye ziwa Tanganyika, mratibu wa kitaifa wa mradi wa usimamizi wa mazingira wa ziwa Tanganyika katika ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mratibu wa kwanza wa Jukwaa la Nishati Tanzania.

Mipango ya mazishi ya Prof. Nkotagu inafanywa na familia ya marehemu kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Roho ya Marehemu Ipumzike kwa Amani!

**Imetolewa na Ofisi ya Uhusiano kwa Umma**  
**31 Agosti 2021**